



SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

"Tunayaangaza maisha yako"



MKATABA WA HUDUMA KWA WATEJA

SHIRIKA LA UMEME TANZANIA



“Tunayaangaza Maisha Yako”

***MKATABA WA HUDUMA
KWA WATEJA***

YALIYOMO

	UKURASA
Tamko la Dira ya Kampuni	3
Tamko la Dhamira ya Kampuni	3
Mambo ya jumla	3
VIWANGO VYA UTOAJI HUDUMA	
KUUNGANISHA UMEME KWA MTEJA	4
Makadirio ya Gharama za kuunganisha Umeme kwa Mteja	4
Kulipia Gharama za Kuunganisha Umeme kwa Awamu	4
Ujenzi wa Njia ya Umeme ya Kumuunganisha Mteja	5
UPIMAJI WA UMEME ANAOTUMIA MTEJA	6
Usomaji wa Mita za wateja	6
Kuhoji Usahihi wa Mita za Matumizi Kabla ya Malipo au Mita za Matumizi Baada ya Malipo	7
Makadirio ya Matumizi ya Umeme	7
Ulipaji wa Bili za Umeme	7
Kukatiwa Umeme Kutokana na Kutolipia Matumizi	8
Maulizo ya Ankara	9
TAARIFA YA KATIZO LA UMEME	9
Utaratibu wa Kutoa Taarifa ya Katizo la Umeme	10
HAKI NA WAJIBU MUHIMU WA MTEJA	11
Haki za mteja	11
Wajibu wa mteja	11
WAJIBU WA TANESCO KWA MTEJA	12
MALALAMIKO, MAULIZO , NA MAOMBI YA MTEJA	
Malalamiko ya Mteja	13
Maulizo ya Mteja	13
Maombi ya Mteja	13
VIAMBATISHO	
Huduma za Simu	14

**TAMKO LA
DIRA YA
KAMPUNI**

Kuwa Kampuni yenye ufanisi na mtazamo wa kibiashara na inayomjali mteja ambayo inaunga mkono maendeleo ya Tanzania na kufikia kiwango cha kuwa muhimili wa uzalishaji nishati ya umeme katika Afrika Mashariki.

**TAMKO LA
DHAMIRA YA
KAMPUNI**

Kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kwa ufanisi na ushindani endelevu kwa namna inavyowezekana.

**MAMBO YA
JUMLA**

Mkataba huu unaweza kurekebishwa katika vipindi tofauti kulingana na mahitaji yatakayojitokeza, na pia kutokana na maoni ya wadau juu ya kuboresha huduma ili kukidhi mahitaji ya wateja.

VIWANGO VYA UTOAJI HUDUMA

A: KUUNGANISHA UMEME KWA MTEJA

1. Makadirio ya gharama za kuunganisha umeme kwa mteja

Kama mteja ameshajaza fomu ya kuomba huduma ya kuungiwa umeme na kuwasilisha viambatisho vyote muhimu vinavyotakiwa (ambavyo ni picha moja na mchoro unaoonyesha nyaya zilivyosambazwa kwenye jengo husika uliosainiwa na kupigwa muhuri na Mkandarasi wa umeme aliyesajiliwa), muda ufuatao wa kupewa makadirio ya gharama utazingatiwa;

- a. Ndani ya siku 7 za kazi iwapo miundombinu iliyopo inaweza kutumika (ndani ya mita 30 kutoka kwenye nguzo iliyo karibu).
- b. Ndani ya siku 10 za kazi kama ujenzi wa njia ya umeme unahitajika (ambao siyo zaidi ya mita 100 kutoka kwenye nguzo iliyo karibu).
- c. Kama mfumo mpya wa usambazaji unahitajika kujengwa, au kama uunganishaji wa mfumo unatakiwa kwa wateja wenye viwanda au biashara kubwa, makadirio yatatolewa ndani ya siku 14 za kazi.

2. Kulipia gharama za kuunganisha umeme kwa awamu

Baada ya kupewa makadirio ya gharama, mteja anayetaka kulipia gharama za kuunganisha umeme kwa awamu ataomba na hatimaye ataingia mkataba na TANESCO wa kulipia gharama hizo kwa awamu.

- a. TANESCO itaruhusu awamu za malipo zisizozidi tatu kwa miezi mitatu mfululizo.
- b. Awamu ya kwanza itajumuisha malipo yote ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

- c. Mteja atakayeshindwa kulipia kiasi chote cha gharama ndani ya miezi mitatu atawajibika kulipa gharama za ziada endapo kutatokea ongezeko la gharama katika kipindi hicho.
- d. Mteja ataunganishiwa umeme baada ya kulipa kiasi chote cha gharama.

3. Ujenzi wa njia ya umeme ya kumuunganisha mteja

Kama mteja amelipa gharama zote anazodaiwa na kama ametimiza wajibu kwa mujibu wa fomu ya maombi ya umeme, na kama pale inapohusika ruzuku zote zimepokelewa na TANESCO, muda ufuatao utazingatiwa katika kutoa huduma ya uunganishaji umeme kwa mteja:

- a. Ndani ya siku 30 za kazi kama miundo mbinu iliyopo inaweza kutumika (ndani ya umbali wa mita 30 kutoka kwenye nguzo iliyo karibu).
- b. Ndani ya siku 60 za kazi kama ujenzi wa njia ya nyongeza unahitajika (hiyo ni kama mteja yuko kati ya mita 30 na mita 100 kutoka kwenye nguzo ya TANESCO iliyo karibu).
- c. Kama mfumo mpya wa usambazaji unahitajika kujengwa, au kama mfumo wa umeme mkubwa unahitajika kuongezwa kwa ajili ya kiwanda au biashara kubwa (kama hakuna mfumo wa kumuunganisha mwombaji) muda wa kumuunganisha mteja utakuwa ndani ya siku 90 za kazi.
- d. Fedha zilizolipwa na mteja kwa TANESCO na kuendelea kuwa mikononi mwa TANESCO kwa zaidi ya muda ulioelezwa hapo juu zitazaa riba ya asilimia 0.5% ya kiasi alicholipia mteja kila siku lakini isizidi asilimia 50% ya gharama.
- e. Endapo TANESCO itashindwa kumuunganishia mteja umeme kwa muda uliotakiwa, TANESCO itawajibika kumtaarifu mteja mapema kuhusiana na hali hiyo, na mteja atafahamishwa ni lini ataunganishiwa umeme.

B: UPIMAJI WA UMEME ANAOTUMIA MTEJA

1. Usomaji wa Mita za Wateja

- a. Wateja wote wanaotumia mita za malipo baada ya matumizi, mita zao zitasomwa angalau mara moja ndani ya miezi miwili (2). Kama mita haitasomwa katika mwezi wowote, matumizi ya mwezi huo yatakadiriwa na marekebisho kama yapo yatafanywa wakati mita itakaposomwa mwezi unaofuata. Wateja wanahimizwa kutoa taarifa kama mita haijasomwa kwa muda wa miezi miwili (2) mfululizo.
- b. Usomaji wa mita wa ziada utafanyika kama mteja anahama kwenye sehemu iliyopo na mteja mwingine anaingia, baada ya kubadilisha mita, au kama mteja atataka mita yake isomwe kwa ajili ya marekebisho ya bili.
- c. Wamiliki wa nyumba/majengo wanaotarajia kubadilisha umiliki au matumizi ya nyumba/majengo yao kama vile kutoka matumizi ya kuishi na kuwa ya biashara lazima watoe taarifa TANESCO angalau siku 30 kabla ya mabadiliko hayo hayajafanyika. Wamiliki wa nyumba/majengo lazima pia watoe taarifa ndani ya kipindi hicho hicho kama wapangaji wao wanatarajia kuhama. Kama mmiliki/wamiliki wa nyumba/jengo husika hawataitaarifu TANESCO kwa kipindi kilichoelezwa hapo juu, wao ndio watawajibika kulipa deni la nyuma ambalo halikulipwa na mpangaji aliyehama.
- d. Kushindwa kutoa taarifa kama ilivyoenezwa hapo juu, na mmiliki/wamiliki kushindwa kulipa deni la nyuma pale mpangaji anapoacha deni, TANESCO ina haki ya kukatisha huduma yake mpaka deni inalodai litakapolipwa kwa ukamilifu kama litakuwepo.

2. Kuhoji Usahihi wa Mita za Matumizi Kabla ya Malipo au Mita za Matumizi Baada ya Malipo

- a. Mteja ana haki ya kudai uchunguzi wa mita.
- b. TANESCO ina wajibu wa kuitikia ombi la mteja la kudai uchunguzi wa usahihi wa mita kama huduma kwa wateja.
- c. Uchunguzi wa usahihi wa mita kwenye eneo la mteja utanza siku tatu (3) za kazi baada ya kupokea ada ya uchunguzi wa mita na matokeo ya uchunguzi yatatolewa kwa mteja ndani ya siku 15 za kazi.
- d. Ada za uchunguzi wa mita zitakuwa kama zilivyoidhinishwa na Mdhhibiti. Ada hizo hazitarudishwa kama mita itagundulika kuwa sahihi. Endapo mita itaonekana kuwa siyo sahihi, ada hiyo itaingizwa kama amana kwenye ankara ya mteja na mteja atapewa marekebisho ya ankara yake kwa maandishi ndani ya siku 7 za kazi.
- e. Mita ambayo itagundulika kuwa siyo sahihi itabadilishwa na marekebisho ya bili yatafanyika ndani ya siku 3 za kazi.

3. Makadirio ya Matumizi ya Umeme

Kama italazimika kukadiria matumizi ya umeme katika kipindi fulani, msingi wa ukadiriaji utakuwa ni usomaji wa mita wa matumizi ya miezi mitatu ya nyuma.

4. Ulipaji wa Bili za Umeme

Kama hakuna masharti mengine yaliyokubaliwa kabla, masharti yafuatayo yatatumiwa;

- a. TANESCO itatoa bili kila mwezi kwa wateja wote wanaotumia mita za matumizi kabla ya malipo.
- b. Kila mteja anawajibika kulipa bili yake ndani ya siku 7 tangu

tarehe ya kutolewa bili husika. Kama mteja hatapokea bili hadi wiki ya mwisho ya mwezi anatakiwa afuatilie bili yake kwenye ofisi za TANESCO.

- c. Iwapo bili haikulipwa katika siku thelathini (30) tangu kutolewa kwa ankara ya madai, itatozwa riba kiasi cha asilimia mbili (2%) kwa mwezi ambao mteja atachelewa kulipa.

5. Kukatiwa Umeme Kutokana na Kutolipia Matumizi

Kama ilivyo katika sheria ya umeme namba 10 ya mwaka 2008 kifungu cha 28; mwenye leseni ya kutoa huduma ya umeme anaweza kukata umeme kwa mteja ambaye atakiuka wajibu wa kimkataba wa kupatiwa huduma ya umeme mpaka hapo atakapolipa deni lake lote la nyuma pamoja na ada ya kurudishiwa umeme. Kwa hiyo:-

- a. TANESCO itakata umeme kwa wateja wote wenye kukiuka utaratibu uliowekwa.
- b. Kukata umeme kutafanyika siku 7 baada ya muda wa malipo ulioelezwa kwenye bili ambao ni sawa na siku 14 baada ya tarehe ya kutolewa bili.
- c. Wateja watapewa taarifa kwa muda ambao siyo pungufu ya masaa 48 kabla ya kukatiwa umeme.
- d. Kukata umeme kutafanyika tu hadi masaa 2 kabla ya muda wa kufunga sehemu za kulipia.
- e. Kukata umeme hakutafanyika siku za mwisho wa wiki au siku za mapumziko ya umma.
- f. Kurudisha umeme kutafanywa mapema iwezekanavyo na siyo zaidi ya siku ya kwanza ya kazi baada ya malipo kamili ya madai ya matumizi na ada ya kurudishiwa umeme.
- g. Kukatiwa umeme kutafanywa siku yoyote ya wiki endapo mteja atagundulika kuwa anaiba umeme kwa njia ya kuchezea mita

au mfumo wake, kutumia umeme bila kupimwa, kujiunganishia umeme baada ya kukatiwa, ama kujiunganishia njia ya umeme au mita ya umeme isivyo halali.

- h. Endapo TANESCO itamkatia umeme mteja kimakosa kwa madai ya kutokulipia matumizi, TANESCO itawajibika kumfidia mteja husika kwa kiwango kilichowekwa kwenye kanuni zilizotungwa na Mdhibiti (EWURA). Kwa muda huu, TANESCO itawajibika kumfidia mteja mara tano (5) ya kiwango cha bei ya umeme ya TANESCO kwa kiasi cha umeme ambacho mteja alikikosa kwa kuangalia matumizi ya mteja kwa siku thelathini (30) zilizopita.

6. Maulizo ya Ankara

- a. Kuhusu Ankara zinazohitaji uchunguzi, maulizo ya Ankara yaliyofanywa na mteja kwa kufika mwenyewe sehemu ya huduma/kituo cha malipo, kwa maandishi au kwa simu, yatafanyiwa kazi na majibu kupendekezwa na kutolewa taarifa ndani ya siku 10 za kazi.
- b. Mteja anawajibika kulipa malipo anayodaiwa bila kujali uchunguzi unaoendelea.

C: TAARIFA YA KATIZO LA UMEME

1. TANESCO itatumia njia muafaka za mawasiliano kuwaeleza wateja wake juu ya katizo la umeme lililopangwa. Taarifa zifuatazo zitatolewa.

- a. Muda ambao katizo limepangwa kutokea.
- b. Maeneo yatakayoathirika
- c. Sababu za katizo la umeme lililopangwa
- d. Muda ambao umeme utarudishwa.

2. Utaratibu wa Kutoa Taarifa ya Katizo la Umeme

- a. Taarifa itatolewa siku 10 kabla ya katizo lililopangwa
- b. Kwa wateja wakubwa, TANESCO na wateja watakubaliana juu ya mpango wa katizo. Kama haitawezekana, TANESCO itatuma taarifa kwa watumiaji wakubwa wa umeme (yaani wateja ambao siyo D1 na T1), kwa maandishi (barua halisi) au kupitia barua pepe.
- c. Kwa katizo la umeme ambalo halikupangwa na ambalo litaathiri sehemu kubwa (ikiwemo kuzimika kwa gridi ya Taifa) TANESCO itaujulisha umma/wateja binafsi sababu za katizo. TANESCO itachagua njia muafaka ya mawasiliano kuwajulisha wateja wake kuhusiana na katizo lolote la umeme ndani ya masaa 24.
- d. Kwa katizo la umeme lisilopangwa kwa mteja mmoja mmoja au maeneo madogo, TANESCO itafanya bidii ya kurudisha umeme ndani ya masaa 24 kutegemeana na aina ya tatizo. Kwa tatizo ambalo haliwezi kurekebishwa ndani ya kipindi hicho kama vile kuanguka kwa nguzo kulikosababishwa na mvua au upepo au kuharibika kwa kifaa kikubwa kutokana na matatizo ya kiufundi, wateja watajulishwa ndani ya kipindi kilichotajwa. Hata hivyo kwa matatizo madogo TANESCO itarudisha umeme ndani ya masaa 12.
- e. Kama italazimika kupunguza matumizi ya umeme kwa mgao wa umeme, maslahi ya taifa yatalindwa kwa kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa umeme kwenye maeneo muhimu na nyeti kama vile Ikulu, Ofisi za Wizara, Mahospitali na vyyuo vikuu. Hivyo, kipaumbele cha kwanza kitabakia kuwa ni kutowakatia umeme wateja hao, isipokuwa kama hali ya umeme haitaruhusu kabisa.

D: HAKI NA WAJIBU MUHIMU WA MTEJA

1. Haki za Mteja

Mteja ana haki za:-

- a. Usahihi wa vipimo vya matumizi ya umeme
- b. Bili zisizo na makosa
- c. Kuhudumiwa kwa heshima
- d. Kupata huduma za kiwango cha juu
- e. Kuhudumiwa vizuri na kwa haraka
- f. Kuhudumiwa kwa usawa
- g. Usiri wa habari zao.
- h. Huduma ya umeme yenye ubora stahiki
- i. Kushirikishwa kwenye mambo yanayowahusu/
yanayowagusa
- j. Kutoa malalamiko

2. Wajibu wa Mteja

Mteja atawajibika:-

- a. Kulipa umeme aliotumia kwa wakati.
- b. Kulinda mali za TANESCO kwenye maeneo yake.
- c. Kulinda mifumo ya TANESCO kutokana na uharibifu wowote ukiwemo wa kiufundi.
- d. Kutoa taarifa kwa TANESCO mapema kabla ya kuhamia kwenye nyumba/jengo.
- e. Kumwomba mmiliki wa eneo analotaka kuhamia kulipia madeni ya eneo husika kabla ya yeye kuingia (TANESCO haitaunga umeme kwenye eneo lenye deni kwa mteja mpya tofauti na aliyekuwepo mpaka deni lote lilipwe).
- f. Atakagua mifumo yake ya ndani kila baada ya miaka mitano kwa kutumia mkandarasi wa umeme aliyesajiliwa ili kubaini

mapungufu ya mifumo ndani ya eneo lake, na hatimaye kuchukua hatua muafaka za marekebisho.

- g. Kulinda mifumo yake ya umeme wa ndani pamoja na vifaa vyote vya umeme vilivyunganishwa baada ya mita.

E: WAJIBU WA TANESCO KWA MTEJA

- a. Wateja wataombwa ushauri kuhusiana na huduma zinazotolewa na TANESCO.
- b. Kuwajulisha wateja kuhusu viwango vya huduma zinazotolewa na TANESCO na wategemee nini kutoka TANESCO kama mtoa huduma.
- c. Kuhudumia wateja
- d. Kuwa waadilifu na wawazi katika kuwahudumia wateja.
- e. Kutoa habari kamili na sahihi kuhusiana na huduma zinazotolewa.
- f. Maboresho endelevu ya huduma kwa kukuza ubunifu na kujifunza.
- g. Wajibu wa TANESCO huishia kwenye mita na wajibu wa mteja huanzia baada ya mita
- h. Kuwafidia wateja pale ambapo tatizo la umeme limesababisha uharibifu wa mali baada ya kuwa imehakikishwa kwamba tatizo hilo halikusababishwa kwa hali yoyote na mtumiaji wa umeme.

F: MALALAMIKO, MAULIZO, NA MAOMBI YA MTEJA

1. Malalamiko ya Mteja.

- a. Malalamiko ya mteja yaliyowasilishwa kwa maandishi yatajibiwa kwa maandishi ndani ya siku 3 za kazi na tatizo litatafutiwa ufumbuzi ndani ya mwezi mmoja (1). Kama tatizo halitaweza kutatuliwa ndani ya mwezi mmoja, mteja atafahamishwa.
- b. Pale ambapo huduma inayotolewa na TANESCO haitamridhisha mteja, mteja anaweza kupeleka malalamiko yake EWURA baada ya kujiridhisha kwamba TANESCO haiwezi kumsaidia.

2. Maulizo ya Mteja

- a. Kama kazi ya uchunguzi inahitajika, maulizo yote kwa njia ya simu au yaliyowakilishwa na mteja mwenyewe kwa kufika ofisini yatajibiwa ndani ya siku 5 za kazi.
- b. Maulizo ya maandishi nayo yatajibiwa ndani ya siku 5 za kazi.
- c. Maulizo yoyote yatatatuliwa ndani ya wiki moja.

3. Maombi ya Mteja

Maombi yote ya mteja yaliyowasilishwa kwa maandishi (kwa mfano kusogeza mita, kubadili mita, kusogeza nguzo, kubadilisha mfumo wa usambazaji), yatajibiwa na TANESCO kwa maandishi ndani ya wiki 2 baada ya kuyapokea. Majibu yatahusisha habari/taarifa kuhusu gharama kwa mteja, wajibu wa mteja na muda wa kutekeleza maombi husika.

Kiambatanisho G1: HUDUMA ZA SIMU

1. Kutoa huduma za simu muhimu

- Huduma za simu za masaa 24 zitatolewa kusaidia kutoa taarifa za hitilafu za umeme na dharura.
- TANESCO itatoa huduma kwa malalamiko, maombi na maulizo. Huduma hii itatolewa wakati wa masaa ya kawaida ya kazi.

MKOA	NAMBA YA SIMU (OFISI)	ANWANI YA BARUA PEPE	FAKSI
Arusha	027-2503552/3	rm.arusha@tanESCO.co.tz	027-2508028
Dodoma	026-2322095	rm.dodoma@tanESCO.co.tz	026-2353040
Coast	023-2402044	rm.coast@tanESCO.co.tz	023-2402141
Ilala	022-2133332	rm.ilala@tanESCO.co.tz	022-2125955
Iringa	026-2702543	rm.iringa@tanESCO.co.tz	026-270-2400
Kagera	028-2220455	rm.kagera@tanESCO.co.tz	028-22-20621
Kigoma	028-2802561	rm.kigoma@tanESCO.co.tz	028-280-2368
Kinondoni North	022-2700364	rm.kinondonin@tanESCO.co.tz	022-2700364
Kinondoni South	022-2170129	rm.kinondonis@tanESCO.co.tz	022-2170170
Kilimanjaro	027-2754035	rm.kilimanjaro@tanESCO.co.tz	027-2751801
Lindi	023-2202840	rm.lindi@tanESCO.co.tz	023-2202840
Manyara	027-2530590	rm.manyara@tanESCO.co.tz	027-2531045
Mara	028-26-22249	rm.mara@tanESCO.co.tz	028-2620221
Mbeya	025-250-3691	rm.mbeya@tanESCO.co.tz	025-2504358
Morogoro	023-2613501/2	rm.morogoro@tanESCO.co.tz	023-2613515
Mtwara	023-2333250	rm.mtwara@tanESCO.co.tz	023-2333651
Mwanza	028-2501021	rm.mwanza@tanESCO.co.tz	028-2501074
Rukwa	025-2800558	rm.rukwa@tanESCO.co.tz	025-2802585
Ruvuma	025-2602621	rm.ruvuma@tanESCO.co.tz	025-2602621
Singida	026-2502892	rm.singida@tanESCO.co.tz	026-2502892
Shinyanga	028-2762120	rm.shinyanga@tanESCO.co.tz	028-2763672

Tabora	026-2604017	rm.tabora@tanESCO.co.tz	026-2604301
Tanga	027-2646781	rm.tanga@tanESCO.co.tz	027-2646777
Temeke	022-2138354	rm.temeke@tanESCO.co.tz	022-2129804
General Manager Marketing	022-2451226	gmm.marketing@tanESCO.co.tz	022-2452042
Managing Director	022-2451159	md.tanESCO@tanESCO.co.tz	022-2451158

HUDUMA ZA DHARURA

MKOA	HUDUMA YA DHARURA – NAMBA YA SIMU
Arusha	027-2503551/2506110
Kagera	028-2220061/3
Dodoma	026-2322095
Ilala	022-2133330, 022-2111044/5
Iringa	026-2702019
Kigoma	028-2802668
Kinondoni North	022-2700358/67
Kinondoni South	022-2171759/66
Lindi	023-2202282
Manyara	027-2530590
Mbeya	025-2504219
Morogoro	023-2613501/2,
Moshi	027-2755007/8
Mtwara	023-2333902
Musoma	028-2622020
Mwanza	028-2500090/1060
Shinyanga	028-2762386/3672
Singida	026-2502133
Songea	025-2602281
Sumbawanga	025-2802097
Tabora	026-2604784
Tanga	027-2646779
Temeke	022-2138352
Coast	023-2402044 / 2402387

WILAYA ZA TANESCO: NAMBA ZA SIMU

TANESCO DISTRICTS	TELEPHONE NUMBERS	DISTRICTS	NUMBERS
KARATU	027-2534251	KILOSA	023-2623038
MBULU	027-2533102	MAHENGE/	023-2620371/
MERERANI	027-2553989	MVOMERO	023-2620029
MONDULI	027-2538044	MASASI	023-2510041
KITETO	027-2552062	NEWALA	023-2410332
KONDOA	026-2321548	TANDAHIMBA	023-2410034
KONGWA	026-2321138	GEITA	028-2520306
MPWAPWA	026-2322155	MAGU	028-2530144
KISARAWA	023-2402850	MISUNGWI	028-2500920
MAFINGA	026-2772015	SENGEREMA	028-2590078
MAKETE	026-2740021	NGUDU	028-2500966
NJOMBE	026-2782317	MPANDA	025-2820197
MAKAMBAKO	026-2730012	TUNDURU	025-2680281
KARAGWE	028-2222996	BARIADI	028-2700180
MULEBA	028-2222689	KAHAMA	028-2710752
HAI	027-2756171	MASWA	028-2750234
HIMO	027-2756229	MEATU	028-2795017
MWANGA	027-2757750	KATESHI	027-2530007
ROMBO	027-2757276	KIOMBOI	026-2502231
SAME	027-2758122	MANYONI	026-2540011
BAGAMOYO	023-2440294	IGUNGA	026-2650096
CHALINZE	022-2129459	NZEGA	026-2692452
KILWA MASOKO	023-2013051	HANDENI	027-2641773
LIWALE	THROUGH TTCL-7	KOROGWE	027-2640566
BUNDA	028-2621225	LUSHOTO	027-2640028
TARIME	028-2690107	BUSHIRI	027-2630071
CHUNYA	025-2520076	MUHEZA	027-2641239
ILEJE	025-2570112	IKWIRIRI	023-2010006
KYELA	025-2540137	MAFIA	023-2010183
MBOZI	025-2580001	KIGAMBONI	022-2820306
TUKUYU	025-2552024	USA RIVER	027-2553628
IFAKARA	023-2625001	MKURANGA	023-2402795
			0784-902391